# 1 Timotheo

*Salamu*

1 Paulo, mtume wa Al-Masihi Isa, kwa amri
ya Mungu Mwokozi wetu, na ya Al-Masihi Isa
aliye tumaini letu.
2 Kwa Timotheo, mwanangu halisi katika
imani.
Neema, rehema na amani zinazotoka kwa
Mungu Baba[*] Mwenyezi na kwa Al-Masihi Isa,
Bwana wetu.

*Maonyo dhidi ya walimu wa uongo*

3 Kama nilivyokusihi wakati nilipoenda Make-
donia, endelea kubaki Efeso, ili upate kuwaagiza
watu wasiendelee kufundisha mafundisho ya
uongo
4 wala wasitoe muda wao kwa hadithi za
kubuniwa na orodha za majina ya vizazi vi-
sivyo na mwisho, ambazo huchochea mabishano
badala ya mpango wa Mungu utokanao na imani.
5 Kusudi la maagizo haya ni upendo unaotoka
katika moyo safi, dhamiri safi na imani ya kweli.
6 Watu wengine wamepotoka kutoka haya na
kugeukia majadiliano yasiyo na maana kwa
kuwa,
7 wanataka kuwa walimu wa Torati, lakini
hawajui mambo yale wanayosema wala hayo
wanayoyatumainia kwa uthabiti.

[*] **1:2** Kwa mwanadamu, Mwenyezi Mungu ni Baba kupitia uhusiano unaopatikana katika kumtumaini Isa Al-Masihi.

8 Tunajua kwamba sheria ni njema ikiwa inatumika kwa halali kama ilivyokusudiwa.
9 Lakini tunajua ya kuwa sheria si kwa ajili ya wenye haki, bali kwa ajili ya wavunja sheria na waasi, kwa ajili ya wasiomcha Mungu na wenye dhambi, wasio watakatifu na wanaokufuru; kwa wale wawauao baba zao au mama zao, kwa wauaji,
10 kwa wazinzi na wahanithi, kwa wale wauzao watu, na kwa waongo na waapao kwa uongo, na kwa chochote kingine kilicho kinyume na mafundisho ya kweli,
11 ambayo yanakubaliana na Injili ya utukufu wa Mungu anayehimidiwa, ambayo mimi nimewekewa amana.

### *Neema ya Mwenyezi Mungu kwa Paulo*

12 Namshukuru Al-Masihi Isa Bwana wetu, aliyenitia nguvu, kwa sababu aliniona mwaminifu, akaniteua kwa kazi yake.
13 Ingawa wakati fulani nilikuwa mwenye kukufuru, mtesaji na mwenye jeuri, lakini nilipata rehema kwa sababu nilitenda hivyo kwa kutojua na kutoamini kwangu.
14 Neema ya Bwana wetu ilimiminwa juu yangu kwa wingi, ikiambatana na imani na upendo ulio katika Al-Masihi Isa.
15 Msemo huu ni wa kweli na unaostahili kukubalika, usemao kwamba: Al-Masihi Isa alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi, ambao mimi ndiye niliye mbaya kuliko wote.
16 Lakini kwa sababu hiyo nilipata rehema, ili katika mimi, niliyekuwa mwenye dhambi kuliko wote, Al-Masihi Isa apate kuonesha uvumilivu

wake usio na kikomo, ili niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini na wapate uzima wa milele.
17 Basi Mfalme wa milele, asiye na mwisho, asiyeonekana, aliye Mungu pekee, apewe heshima na utukufu milele na milele. Amen.

### *Timotheo anaagizwa upya*

18 Mwanangu Timotheo, ninakupa agizo hili, kwa kadiri ya maneno ya unabii yaliyosemwa kukuhusu, ili kwa kuyafuata upate kupigana vita vizuri,
19 ukiishikilia imani na dhamiri safi, ambazo wengine wamevikataa, na hivyo wakaangamia kwa habari ya imani yao.
20 Miongoni mwao wako Himenayo na Iskanda, ambao nimemkabidhi Shetani ili wafundishwe wasije wakakufuru.

# 2

### *Maagizo kuhusu ibada*

1 Awali ya yote, nasihi kwamba dua, sala, maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote:
2 kwa ajili ya wafalme na wale wote walio katika mamlaka, ili tupate kuishi kwa amani na utulivu, katika uchaji wote wa Mungu na utakatifu.
3 Jambo hili ni jema, tena linapendeza machoni pa Mungu Mwokozi wetu,
4 anayetaka watu wote waokolewe na wafikie kuijua kweli.
5 Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani mwanadamu Al-Masihi Isa,

6 aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya
wanadamu wote: jambo hili lilishuhudiwa kwa
wakati wake ufaao.
7 Nami kwa kusudi hili nimewekwa niwe
mhubiri na mtume (nasema kweli katika Al-
Masihi wala sisemi uongo), mwalimu wa watu
wa Mataifa katika imani na kweli.
8 Nataka kila mahali wanaume wasali waki-
inua mikono mitakatifu pasipo hasira wala ku-
gombana.
9 Vivyo hivyo nataka wanawake wajipambe
kwa adabu na kwa heshima katika mavazi
yanayostahili, si kwa kusuka nywele, kuvalia
dhahabu, lulu au mavazi ya gharama kubwa,
10 bali kwa matendo mazuri kama iwapasavyo
wanawake wanaokiri kuwa wanamcha Mungu.
11 Mwanamke na ajifunze katika utulivu na
utiifu wote.
12 Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha
au kuwa na mamlaka juu ya mwanaume.
Mwanamke inampasa kukaa kimya.
13 Kwa maana Adamu aliumbwa kwanza, kisha
Hawa.
14 Wala si Adamu aliyedanganywa, bali ni
mwanamke aliyedanganywa akawa mkosaji.
15 Lakini mwanamke ataokolewa kwa kuzaa
kwake, wakiendelea kudumu katika imani, up-
endo na utakatifu, pamoja na kuwa na kiasi.

# 3

*Sifa za waangalizi*

1 Hili ni neno la kuaminiwa, kwamba mtu aki-
tamani kuwa mwangalizi wa kundi la waumini,
atamani kazi nzuri.

2 Basi, imempasa mwangalizi awe mtu asiye
na lawama, mume wa mke mmoja, mwenye
kiasi, anayejitawala, anayeheshimika, mkarimu,
ajuaye kufundisha,
3 asiwe mlevi, wala mkali bali awe mpole,
asiwe mgomvi wala mpenda fedha.
4 Lazima aweze kuisimamia nyumba yake
mwenyewe vizuri na kuhakikisha kwamba wa-
toto wake wanamtii na kuwa na heshima kwa
kila njia.
5 (Kwa maana kama mtu hajui jinsi ya kusi-
mamia nyumba yake mwenyewe, atawezaje ku-
liangalia kundi la waumini la Mungu?)
6 Asiwe mtu aliyeongoka karibuni asije aka-
jivuna na kuangukia kwenye hukumu ile ile ya
ibilisi.
7 Inampasa pia awe na sifa njema kwa watu
walio nje, ili asije akalaumiwa na kuanguka
kwenye mtego wa ibilisi.

### *Sifa za mashemasi*

8 Vivyo hivyo, mashemasi nao wawe watu
wanaostahili heshima, wasiwe wenye kauli mbili
au wenye kujifurahisha kwa mvinyo, wala
wanaotamani faida isiyo halali.
9 Inawapasa kushikamana sana na ile siri ya
imani kwa dhamiri safi.
10 Ni lazima wapimwe kwanza; kisha kama
hakuna neno dhidi yao, basi na waruhusiwe
kuhudumu kama mashemasi.
11 Vivyo hivyo, wake zao wawe wanawake
wanaostahili heshima, wasio wasingiziaji, bali
wawe na kiasi na waaminifu katika kila jambo.

12 Shemasi awe mume wa mke mmoja, na aweze kusimamia watoto wake na watu wa nyumbani mwake vyema.
13 Wale ambao wamehudumu vyema katika huduma ya ushemasi hujipatia msimamo bora na ujasiri mkubwa katika imani yao ndani ya Al-Masihi Isa.
14 Ingawa ninatarajia kuja kwako hivi karibuni, ninakuandikia maagizo haya sasa ili,
15 nikikawia, utajua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, ambayo ndiyo jumuiya ya waumini ya Mungu aliye hai, iliyo nguzo na msingi wa kweli.
16 Bila shaka yoyote, siri ya utauwa ni kubwa:
Alidhihirishwa katika mwili,
akathibitishwa kuwa na haki katika Roho wa Mungu,
akaonekana na malaika,
akahubiriwa miongoni mwa mataifa,
akaaminiwa ulimwenguni,
akachukuliwa juu katika utukufu.

# 4

*Maagizo kwa Timotheo*

1 Roho wa Mungu asema waziwazi kwamba katika siku za mwisho baadhi ya watu wataiacha imani na kufuata roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani.
2 Mafundisho kama hayo huja kupitia kwa waongo ambao ni wanafiki, hali dhamiri zao zikiungua kwa kuchomwa moto.
3 Wao huwakataza watu wasioe na kuwaagiza wajiepushe na vyakula fulani, ambavyo Mungu

aliviumba ili vipokewe kwa shukrani na wale wanaoamini na kuijua kweli.
4 Kwa maana kila kitu alichokiumba Mungu ni chema, wala hakuna kitu chochote cha kukataliwa kama kikipokewa kwa shukrani,
5 kwa sababu kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba.

### *Mtumishi mwema wa Isa Al-Masihi*

6 Ukiwakumbusha ndugu mambo haya, utakuwa mtumishi mwema wa Al-Masihi Isa, uliyelelewa katika kweli ya imani na yale mafundisho mazuri uliyoyafuata.
7 Usijishughulishe kamwe na hadithi za kipagani na masimulizi ya uongo ya wanawake wazee; badala yake, jizoeze kuwa mtauwa.
8 Kwa maana mazoezi ya mwili yana faida kwa sehemu, lakini utauwa una faida katika mambo yote, yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa na ya ule ujao.
9 Hili ni neno la kuaminiwa tena lastahili kukubaliwa kabisa.
10 Nasi kwa ajili ya hili tunajitaabisha na kujitahidi, kwamba tumeweka tumaini letu kwa Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote, hasa wale waaminio.
11 Mambo haya yaagize na kuyafundisha.
12 Mtu yeyote asikudharau kwa kuwa wewe ni kijana, bali uwe kielelezo kizuri kwa waumini katika usemi, mwenendo, upendo, imani na usafi.
13 Fanya bidii kusoma Maandiko hadharani, kuhubiri na kufundisha, hadi nitakapokuja.

14 Usiache kutumia kipawa kilicho ndani yako,
ambacho ulipewa kwa neno la unabii wakati
wazee walikuwekea mikono.
15 Uwe na bidii katika mambo haya; ujitolee
kwa ajili ya mambo haya kikamilifu, ili kila mtu
aone kuendelea kwako.
16 Jilinde sana nafsi yako na mafundisho yako.
Dumu katika hayo, kwa maana kwa kufanya hivyo, utajiokoa wewe mwenyewe pamoja na wale wanaokusikia.

# 5

*Maagizo kuhusu wajane, wazee na watumwa*

1 Usimkemee mzee kwa ukali bali umshawishi
kama vile angekuwa ni baba yako. Uwatendee vijana kama vile ndugu zako;
2 nao wanawake wazee uwatendee kama
mama zako, na wanawake vijana kama dada zako, katika usafi wote.
3 Waheshimu wanawake wajane ambao ni wa-
jane kweli kweli.
4 Kama mjane ana watoto ama wajukuu, hawa
inawapasa awali ya yote wajifunze kutimiza wajibu wao wa kumcha Mungu katika matendo kwa kuwatunza wale wa jamaa zao wenyewe, na hivyo wawarudishie wema waliowatendea wazazi wao, kwa kuwa hivi ndivyo inavyompendeza Mungu.
5 Mwanamke ambaye ni mjane kweli kweli,
yaani yeye aliyebaki peke yake huweka tumaini lake kwa Mungu naye hudumu katika maombi usiku na mchana akimwomba Mungu ili amsaidie.

6 Lakini mjane aishiye kwa anasa amekufa,
ingawa anaishi.
7 Wape watu maagizo haya pia, ili asiwepo
yeyote wa kulaumiwa.
8 Kama mtu hawatunzi wale wa jamaa yake,
hasa wale wa nyumbani mwake mwenyewe,
ameikana imani, tena ni mbaya kuliko yeye
asiyeamini.
9 Mjane yeyote asiwekwe kwenye orodha ya
wajane isipokuwa awe ametimiza umri wa mi-
aka sitini, na amekuwa mke wa mume mmoja;
10 awe ameshuhudiwa kwa matendo yake
mema, aliyewalea watoto wake vizuri, aliye
mkarimu, aliyewanawisha watakatifu miguu,
aliyewasaidia wenye shida na aliyejitolea kwa
ajili ya matendo mema ya kila namna.
11 Lakini kwa habari za wajane vijana usi-
waweke kwenye orodha hiyo, maana tamaa zao
za kimaumbile zikizidi kule kujitoa kwao kwa Al-
Masihi, watataka kuolewa tena.
12 Nao kwa njia hiyo watajiletea hukumu kwa
kukiuka ahadi yao ya kwanza.
13 Zaidi ya hayo, wajane kama hao huwa
na tabia ya uvivu wakizurura nyumba kwa
nyumba, wala hawawi wavivu tu, bali pia
huwa wasengenyaji, wajiingizao katika mambo
yasiyowahusu na kusema mambo yasiyowapasa
kusema.
14 Hivyo nawashauri wajane vijana waolewe,
wazae watoto na wasimamie nyumba zao, wasije
wakampa adui nafasi ya kutushutumu.
15 Kwa maana kwa kweli wajane wengine
wamepotoka ili kumfuata Shetani.

16 Lakini kama mwanamke yeyote aaminiye
ana wajane katika jamaa yake, inampasa awa-
saidie wala si kuwaacha wakililemea kundi la
waumini, ili lile kundi liweze kuwasaidia wale
ambao ni wajane kweli kweli.

### *Wazee wa kundi la waumini*

17 Wazee wa kundi la waumini wanaoongoza
shughuli za kundi hilo vizuri wanastahili hes-
hima mara mbili, hasa wale ambao kazi yao ni
kuhubiri na kufundisha.
18 Kwa maana Maandiko husema, "Usim-
funge maksai kinywa apurapo nafaka," tena,
"Mfanyakazi anastahili mshahara wake."
19 Usiendekeze mashtaka dhidi ya mzee
isipokuwa yawe yameletwa na mashahidi wawili
au watatu.
20 Wale wanaodumu katika dhambi uwakemee
hadharani, ili wengine wapate kuogopa.

21 Ninakuagiza mbele za Mungu na mbele za
Al-Masihi Isa na mbele za malaika wateule, shika
maagizo haya pasipo ubaguzi wala upendeleo.

22 Usiwe na haraka kumwekea mtu mikono
wala usishiriki dhambi za watu wengine. Jilinde
nafsi yako uwe safi.

23 Acha kunywa maji peke yake, tumia divai
kidogo kwa sababu ya tumbo lako na maumivu
yako ya mara kwa mara.

24 Dhambi za watu wengine ni dhahiri nazo
zinawatangulia kwenda hukumuni; na dhambi
za watu wengine zinawafuata nyuma yao.
25 Vivyo hivyo, matendo mema yako dhahiri,
na hata yale yasiyo dhahiri hayawezi kufichika.

# 6

*Watumwa*

1 Wale wote walio chini ya nira ya utumwa
inawapasa kuwahesabu mabwana zao kuwa
wanastahili heshima yote, ili jina la Mungu lisi-
tukanwe wala mafundisho yetu.
2 Wale watumwa ambao wana mabwana
waaminio, haiwapasi kupunguza heshima yao
kwa sababu wao ni ndugu. Badala yake, wawa-
tumikie hata vizuri zaidi, kwa sababu wale
wanaonufaika na huduma yao ni waumini, am-
bao ni wapendwa wao. Fundisha mambo haya
na uwahimize kuyafuata.

*Mafundisho ya uongo na utajiri wa kweli*

3 Ikiwa mtu yeyote atafundisha mafundisho
mapotovu wala hakubaliani na mafundisho
manyofu ya Bwana wetu Isa Al-Masihi na yale ya
utauwa,
4 huyo anajivuna wala hajui kitu chochote.
Yeye amejaa tamaa ya mabishano na ugomvi
kuhusu maneno ambavyo matokeo yake ni wivu
na mapigano, maneno ya ukorofi, shuku mbaya,
5 na kuzozana kusikokoma kati ya watu walio-
haribika akili zao, walioikosa kweli, na ambao
hudhani kwamba utauwa ni njia ya kupata faida.
6 Lakini utauwa na kuridhika ni faida kubwa.
7 Kwa kuwa hatukuja humu duniani na kitu
chochote, wala hatuwezi kutoka humu na kitu.
8 Lakini kama tuna chakula na mavazi, tutarid-
hika navyo.
9 Lakini wale watu wanaotamani kuwa na
mali kwa haraka huanguka kwenye majaribu,
na wamenaswa na tamaa nyingi za kipumbavu

zenye kudhuru, zinazowazamisha watu katika uharibifu na maangamizi.
10 Kwa maana kupenda fedha ndiyo shina moja la maovu ya kila namna. Baadhi ya watu wakitamani fedha, wameiacha imani na kujichoma wenyewe kwa maumivu mengi.

### *Mambo mazuri ya imani*

11 Lakini wewe, mtu wa Mungu, yakimbie mambo haya yote. Fuata haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole.
12 Pigana vile vita vizuri vya imani. Shika uzima wa milele ambao ndio ulioitiwa ulipokiri ule ukiri mzuri mbele ya mashahidi wengi.
13 Nakuagiza mbele za Mungu avipaye vitu vyote uhai, na mbele za Al-Masihi Isa, ambaye alipokuwa anashuhudia mbele ya Pontio Pilato alikiri ukiri mzuri,
14 uishike amri hii bila dosari wala lawama hadi kufunuliwa kwake Bwana wetu Isa Al-Masihi;
15 ambako Mungu atadhihirisha kwa wakati wake mwenyewe: Mungu ahimidiwaye, aliye peke yake Mtawala, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana,
16 yeye pekee aishiye milele, anayedumu katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye milele. Amen.
17 Waagize wale ambao ni matajiri wa ulimwengu huu waache kujivuna, wala wasiweke tumaini lao katika mali ambayo si ya hakika, bali waweke tumaini lao katika

Mungu ambaye hutupatia vitu vyote kwa wingi ili tuvifurahie.
18 Waagize watende mema, wawe matajiri katika matendo mema, pia wawe wakarimu na walio tayari kushiriki mali yao na wengine.
19 Kwa njia hii watajiwekea hazina kama msingi kwa ajili ya wakati ujao na hivyo watajipatia uzima, yaani ule uzima ambao ni wa kweli.

### *Maelekezo ya binafsi na maombi ya baraka*

20 Timotheo, linda kile kilichowekwa amana kwako. Epuka majadiliano yasiyo ya utauwa na mabishano ambayo kwa uongo huitwa elimu,
21 ambayo wengine kwa kujidai kuwa nayo wameiacha imani.

Neema iwe nanyi. Amen.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: “Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible.” Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d